**Learning by Ear 2009**

**Media & Information**

**Author: Hope Azeda**

**Redaktion: Ludger Schadomsky**

**Kisuaheli Translation: Eric Ponda**

**EPISODE 10**

| *CHARACTERS* | |
|---|---|
| Announcer: | Male/female |
| "Young Junior" | Male, 15 years old |
| "Sister P." | Female, 16 years old |
| "Charlie" | Male, 18 years old |
| "Ezra": | Male, 22 years old. Brother to "Young Junior". |

**INTRO**

Hujambo na kwa mara nyingine karibu kwa makala haya ya 10 na ya mwisho ya mfululizo wa vipindi vyetu vya Learning By Ear kuhusu uandishi wa Habari na Vyombo vya Habari. Kugusia tu yale yaliyotokea wakati wa kipindi kilichotangulia, Charlie, Young P na Sister P wamepata ofisi na kujenga studio baada ya kupata Leseni ya kaunzisha kituo chao cha Redio. Sasa wako tayari kuanza kupeperusha matangazo kupitia stesheni yao mpya. Suala la vianzo

vya habari pia limetatuliwa. Mbali na hayo Ezra amfanikiwa kuwashawishi wandishi wenzake wa Habari kutoka Africa kuchangia katika ripoti kwa shirika la habari la Africa linaloaminika litakuwa tegemeo kubwa kama chanzo cha habari katika stesheni ya Dot.Com. Mambo sasa yanakwenda kama yalivyopangwa, au sivyo?

**SCENE ONE**

**The radio station.**

| **SFX Soft music in the background. Noise of rattling CD covers.** |
|---|

1. Young J: Charlie, Chunga!. Usije ukachanganya hizo CD kwani itakuwa kazi ngumu tena kuzipanga badaye.
2. Charlie: Usiwe na wasi wasi Young J. najaribu kukurahisishia kazi. Napanga na kuhifadhi muziki wote kwa katika Komputa.
3. Young J: Sawa kabisa. Kwa hivyo tayari imefungua ukurasa wa muziki wa Rege, Hip-hop, R&B na ……
4. Charlie: Ndo…! na, sasa unachohitaji kufungua wa komputa na kucheza muziki utakao.
5. Young J: Yo yooo yooo!, Stesheni ya Dot.Com itaanza kutingisha hivi punde.
6. Charlie: Bado siamini, Young J..!, yaani tutakuwa hewani hivi punde na kusikilizwa na maelfu ya watu! Mtu

anapofanya jambo zuri huchukuliwa kuwa ni Malaika!.

7. Young J: Na pia unapofanya jambo la upuzi ulimwengu wote utakuchukia. Kwa kweli hofu yangu kubwa ni kuhusu idadi ya wasichana watakaoanza kunipenda.

8. Charlie: Usiniambie mambo hayo!. Nataka kutoka kidogo!. **SFX Footsteps.** Wakati ninaposhikwa mchecheto huenda chooni kila baada ya dakika tano.

**SFX: Door opening and closing**

9. Young J: (**laughs and talking to someone in the distance)** Bora ujizuiE, kwasababu hutatakuwa na muda wa kwenda chooni mara kwa mara punde tu utakapoanza kwenda hewani.

**SFX: Door opening.**

10. Sister P: Unasema nani?

11. Young J Hee…hehe , Sister P, Umependeza. Nani mwenye bahati usiku wa leo ?

12. Sister P: Young J, wacha kunitania. Kwani unasahau kuwa leo ni siku ya kwanza matngazo yetu kwenda hewani.?

**SFX:Door opening and closing.**

13. Charlie: Haha! Sister P, Kweli umependeza

4. Sister P: Wenzangu siku ya leo ni siku muhimu sana maishani. Nashangaa kumuona mumevalia kama watu wanaokwenda katika shamba la ndizi.

15. Young J: (**laughs)** Lakini hii ni redio sio televisheni, Au bado fikra zako ziko katika kipindi chako cha Televishen "*The Me in Me"*?

16. Sister P: Sawa tosha tosha.

17. Charlie: Lakini nani atakuwa wa kwanza kwenda hewani?

| **SFX Door opening and closing.** |
|---|

18. Sister P: Habari Ezra!.

19. Ezra : Ni nzuri , Sister P.Kweli umevalia nadhifu!.Kwani leo kunamashindano ya urembo au ni kwasababu ya uzinduzi wa stesheni yetu. Je nyote mko tayari kwenda hewani?

22. Charlie: Ndio, lakini bado hatujaamua nani takayeanza!

23. Sister P: Mimi na Young J .

24. Ezra: Tayari mume tayarisha vipindi vyenu ?

25. Young J: Muziki moto moto kabisa. "***Tumpa tumpa tumpa tumpampa".*** Stesheni ya taifa haina muziki moto

moto kama yetu. Nani sasa atakuwa akisikiliza redio hiyo?

6. Sister P: Wako wengi hasa mababu zetu bila shaka.

27. Charlie: Ezra, punde tu redio Dot.Com FM ikianza matangazo yake, nakuomba tafadhali uende barabarani kupata maoni ya watu kuhusiana na matangazo yetu.

28. Ezra: Lakini pia unaweza kupata maoni ya wasikilizaji kupitia vipindi vyenu. Kwa kuwa tayari mumeanza kupeperusha matangazo , ningependa kuwakumbusha mambo fulani.

29. Charlie: Kuhusu nini Ezra?

30. Ezra: Kuwakumbusha kwamba redio ni chombo muhimu chenye uwezo mkubwa sana. Inafikia mamilioni ya watu kwa wakati mmoja.

31. Young J: Kwa hivyo?

32. Ezra: Lazime muwe makini wakati munapotumia chombo hiki. Kusimamia stesheni ni sawa na kuvuka mto. Unaweza kuvuka salama au unapokosea kidogo tu ukazama na mamilioni ya watu wanaokutegemea.

33. Sister P: Ezra, lini ulianza kuzungumza kwa mafumbo kama mtume?. Nieleze wazi wazi unamaanisha nini.

34. Ezra: Ninachomaanisha ni kwamba redio ni nzuri lakini pia athari zake ni kubwa hasa wakati unapokuwa hewani.

35. Charlie: Kumaanisha?.

36. Ezra: Yaani ukitumia redio kama chombo cha uchochezi hapo unahatarisha umma.Unapotoa habari ambazo hazijafanyiwa utafiti au kuthibitishwa pia ni hatari kubwa.

37. Sister P: Kwa ufupi Ezra anatushauri kamba ni lazima tudumishe maadili ya uandishi wa habari la sivyo tutaangamia…Sawa?

38. Ezra: Tumeelewa , Sister P.

39. Sister P: Sasa tutafanya nini punde stesheni hii itakapoanza kupeperusha matangazo yake?. Tuandae karamu ya kukata na shoka kusherehekea ufanisi wetu? Au tujipe muda wa kutafakari mafanikio haya? Tufanye nini katika siku kama ya leo?

END SCENE

**SCENE TWO**

**In the studio**

**SFX hot music is playing**

40. Young J: Natumai unaendelea kufuahia muziki moto moto kutoka stesheni uipendayo ya Dot.Com FM sterioooooo… Mtangazaji wako ni Young J tuwe pamoja!.

41. Sister P: Na kwa wale amabo ndio mwanzo mnafungulia redio zenu, hii ni stesheni mpya ya jamii inayojulikana ..…

42. Young J: Dot.Com FM na nyuma ya Mikrofoni ni mtangazaji wako Young J pamoja na mwezangu…

43. Sister P: Sister Patricia… au unaweza kuniita Sister P.Tuko tayari kuwaporomoshea vibao moto moto na habari zinazochipuka kila baada ya saa moja.…

44. Young J: …Na pia vipindi vya kuelimisha.

45. Sister P: Kwa habari za kuaminika za humu nchini na ulimwengu mzima. Endelea kusikiliza Dot.Com.

| **SFX music for thirty seconds.** |
|---|

46. Sister P: Tumekuahidi muziki moto moto na sasa ni wajibu kutimiza ahadi hiyo.Ukiwa shambani, sokoni au mahali popote sikiliza redio Dot Com.

Young J, kwanini usiwaeleza wasikilizaji kuhusu vipindi tulivyowaandalia?.

47. Young J: Muhimu ni kwamna redio Dot Com ni redio ya jamii kwa ajili yako. Unaweza kutuma maoni kuhusu jinsi ya kuboresha stesheni hii nasi tutafurahi kuyapokea. Kwa habari ,mahojiano na mengi tu kuhusu filamu zinazoonyeshwa katika kumbi mbali mbali sikiliza redio Dot.Com!

Lakini kwanza ni habari za humu nchini mukisomewa na Sister P….. Usikose kusikiliza habari zetu ufahamu yanayoendelea humu nchini na hata ulimwengu mzima kwa jumla….! na yote ni kupitia redio Dot.Com.

48. Sister P: Pia tuna matangazo ya kibiashara nay ale ya kibinafsi.Masuala ya kijamii kama vile mjadala kuhusu ujenzi wa barabara zilizokwama miongo kadhaa iliyopita, redio Dot Com inakupa wewe msikilzaji fursa hiyo ya kutoa maoni. Na kama munavyofahamu kampeni za uchaguzi ujao zinakaribia. Tutawaangazia na kuhojiana moja kwa moja na wanasiasa ili kukupa nafasi wewe msikilizaji kuwauliza maswali.

Pia tunavipindi kuhusu masuala ya mazingira, haki za binadamu, Kilimo na kadhalika, kwa hivyo usikose kusikiliza kituo hiki kipya cha Dot Com. Tutarejea baada ya muda mfupi.

| **SFX Reggae Music** |
| --- |

**SCENE THREE**

**A bar**

**SFX general noise, voices, music in the background**

50. Ezra : Unajisikiaje., ikiwa hii ni mara yako ya kwanza kuwa hewani?

51. Charlie: Nasikia furaha isio na kifani.

52. Young J: Sasa mchecheto wa kwenda chooni kila mara umekwisha?

53. Charlie: Sijui wasi wasi huo wote umeishia wapi. Ghafla wasi wasi wote umenitoka.

**Sfx Glass falling and breaking from a distance.**

54. Ezra: Ni nini hicho, watu wanapigana.?

55. Young J: Hata nafikiri ni mhudumu ameangusha glasi.

56. Sister P: Wenzangu sasa najisikia vizuri sana. Nilitamani kuona siku hii ya leo. Na je kipindi chetu cha kwanza kilikwendaje Ezra…., kipindi kilikuwaje?

57. Ezra: Kilikuwa kizuri sana, nahakika mtafanya kazi nzuri zaidi.

58. Young J: Sister P, Ulifanya uamuzi wa busara kuja apa badala ya kuhudhuria ile karamu.Huu ni wakati

mzuri wa kutafakari mafanikio yetu baada ya kazi ngumu.

59. Sister P: Huwezi kuamini kuwa watu wengi wanaosikiliza stesheni hii.

**Sfx bottles and glasses.**

60. Waitress: Uliagizia vinywaji?

61. Young J: Ndio.

**SFX Opening bottles and pouring sounds**

62. Sister P: Tunamshukuru sana Ezra kwa ushauri wake muhimu na kutuunga mkono wakati wote huo. Ezra unahitaji shukrani zaidi kuliko soda… lakini…..

63. Ezra: Usijali kuhusu suala hilo,pongezi kwa juhudi za kila mmoja wenu. Bila shaka tutanufaika zaidi na ufanisi huu.

**OUTRO**

Waandishi wetu wa habari wamefaulu kuanzisha kituo cha redio na sasa wameanza kuihudumia jumiii. Bila shaka ilikuwa njia ndefu yenye panda shuka nyingi, mbali na vishawishi kutoka kwa wanasiasa.
Ukiwa na maoni kuhusu vipindi vyetu vya Learning By Ear usisite kututumia nasi hapa Bonn tutayapokea. Na

endapo umekosa kusikiliza au ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki,kutembelea mtandao wetu dw-world.d e/lbe.

Hadi tutakapoungana nawe tena wakati mwengine kwaheri kwa sasa.!

THE END